

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

**SHULE YA SEKONDARI ANGAZA,**

**S.L.P 510,**

**LINDI**

**TAREHE...../...../ .....**

**SIMU: 0783329791**

**KUMB: NA ANGSSS/J. INSTR/VOL 1/9**

**MZAZI/MLEZI WA .....**

**YAH: KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA ANGAZA  
MANISPAA YA LINDI MWAKA 2021.**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ANGAZA mwaka 2021. Shule ya Sekondari ya Angaza ipo umbali wa kilometra 04 toka mjini Lindi. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Na unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe 11/01/2001 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021. Baada ya hapo msako wa wanafunzi ambao hawajari poti utafanyika na mzazi ambaye hajamleta mtoto wake shulenii atachukuliwa hatua kali za kisheria dhidi yake. , ikiwa ni kulipa faini au kifungo au vyote kwa pamoja.

**ELIMU NI MWANGA.**

.....  
**LAUSI J. MCHOPA  
MKUU WA SHULE YA SEKONDARI  
ANGAZA**

**MAHITAJI YA SHULE KWA WOTE.**

**1. VIFAA KWA WOTE**

- I. Ndoo 1
- II. Jembe 1 **KUBWA (NGWAMBA)** lenye mpini
- III. Paspoti size 4, ukiwa umevaa sare ya shule.
- IV. Kamusi ya kiingereza / Kiswahili LAZIMA.
- V. Raba za michezo
- VI. Bukuta moja, T.shirt moja, ya michezo rangi ya bluu (**ISIWE NA MAANDISHI YOYOTE**)
- VII. Begi la kubeba madaftali yake.
- VIII. Madaftari makubwa 15 (counter book quire 2)
- IX. Peni za kutosha
- X. Mkebe 1 (mathematical set)
- XI. File moja la kuhifadhi mitihani yake anayofanya shulen. (atabakia nalo mwanafunzi mwenyewe). **LIWE LA PLASTIKI**
- XII. Kalikuleta ndogo moja isiyo ya kisayansi. Itamsaidia kwenye masomo ya sayansi.

## 2. SARE ZA SHULE KWA WASICHANA

- I. Mashati meupe ya mikono mifupi mawili (aina ya tomato)
- II. Sketi mbili (2) rangi ya kitambaa ni kijani cha mgomba pia imeambatanishwa na fomu hii
- III. Viatu vyeusi nya ngozi visivyo na kisigino kirefu wala madoido jozi mbili (2)
- IV. Sokisi nyeupe jozi mbili zisizo na urembo wa aina ye yote
- V. Skin tight nyeusi na track suit rangi ya bluu itatumika wakati wa michezo tu
- VI. Hijabu na nusu kanzu nyeupe iwe ni yenyeye kuhifadhi kwa wanaohitaji na sio ya kubana. Kitambaa cha hijabu na nusu kanzu kiwe cha tetroni na sio cha mpira kinachovutika.

## 3. SARE ZA SHULE KWA WAVULANA

- I. Mashati meupe ya mikono mifupi mawili (aina ya tomato)
- II. Suruali mibili rangi ya kitambaa imeambatanishwa na fomu hii (kijani cha mgomba), iwe na linda mbili. **MODO HAZIRUHUSIWI** chini ishonwe cm 19. (NB marufuku kuva suruali chini ya amakalio/mlegezo)
- III. Viatu nya ngozi vyeusi nya kudumbukiza jozi mbili (2)
- IV. Soksi nyeupe jozi mbili zisizo na urembo wa aina ye yote.
- V. Mkanda wa ngozi wa rangi nyeusi.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATION TRAINING**  
**ANGAZA SECONDARY SCHOOL**  
**P.O.BOX 510**  
**LINDI**

**REF:**

**NO.....**

**THE MEDICAL OFFICE .....**

**RE; REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF**

**MR/MS.....**

Please examine the above named pupil and give us report regarding his/her suitability for secondary school studies.

- I. Pupil's name .....
- II. Blood .....
- III. Stool .....
- IV. T. B Test .....
- V. Syphilis test .....
- VI. Urine .....
- VII. Eye test .....
- VIII. Chest .....
- IX. Ears .....
- X. Spleen .....
- XI. Abdomen .....
- XII. Pregnancy (girls only).....

I certify that the above pupil is suitable /unsuitable for studies.

Give

reason.....

.....

.....

Name of medical officer .....

**HALMASHAURI YA MANISPAAA YA LINDI  
SHULE YA SEKONDARI ANGAZA  
SHERIA ZA SHULE.**

Zifuatazo ni sheria za shule kinyume nazo kutasababisha mwanafunzi kuadhibiwa , kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule kabisa.

**A. MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE:**

- I. Uasherati, ubakaji na ushoga.
- II. Ulevi, uvutaji wa bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.
- III. Kupiga au kupigana
- IV. Kuharibu makusudi mali ya shule/umma
- V. Kudharau bendera ya Taifa
- VI. Kuoa au kuolewa
- VII. Kupata au kusababisha mimba na kutoa mimba ndani au nje ya shule
- VIII. Kugoma na kuchochea au kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu na mali zao.
- IX. Kukataa adhabu
- X. Wizi
- XI. Kunyanyasa wanafunzi wenzake
- XII. Kumiliki au kutumia simu shuleni
- XIII. Kutoka nje ya shule bila kibali maalumu cha mwalimu wa zamu au mkuu wa shule

**B. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI  
KUADHIBIWA**

- I. Kutosimama na kusalimia mwalimu au mtu yejote anayemzidi umri anapopita, kuingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano na mahali pengine popote.
- II. Kuva viatu vyovoyote vyenye mikanda ikiwemo kandambili (ndala) shuleni.
- III. Kutumia lugha chafu dhidi ya wanafunzi wenzake, kwa walimu au mtu mwimgine yejote.
- IV. Kutokuvaa sare sahihi mfano modal trousers
- V. Kutowaheshimu wafanyakazi waliopo shuleni kama walezi wake
- VI. Kutoonesha dhamira ya kushirikiana kazi kwani kazi ni kielelezo cha utu.
- VII. Kutoheshimu au kutothamini kazi za aina zote zinazotolewa na uongozi wa shule
- VIII. Uvutaji sigara
- IX. Kutokunyoa ndevu

- X. Kuvaavu ya mavazi yasiyokuwa na heshima
- XI. Kutotii kengele au kushindwa kuitikia wito wa kiongozi aliyemwita
- XII. Kutoheshimu picha za viongozi wa serikali, nembo ya taifa, wimbo wa taifa na fedha za taifa, kutosimama katika utaratibu maalumu wakati wa kupokea huduma.
- XIII. kutohudhuria vipindi vya madarasani mda wote wa masomo
- XIV. kutoheshimu na kutokubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni
- XV. kutohudhuria kazi zote za mikono, mikutano yote ya shule, ukaguzi na usafi na kupandisha bendera ya Taifa.
- XVI. Kushindwa kudhamini muda
- XVII. Kutowahi kazi zote kama zilivyopangwa ukiwemo wito wa dharura
- XVIII. Kutovaa sare za shule katika sehemu zifuatazo; -
  - a. Drasani
  - b. Shughuli za shule nje ya shule
  - c. Mhadhara wa shule (school baraza)
  - d. Kwenda kutibiwa hospital
  - e. Kwenye maandalimanu yaliyo rasimi
  - f. Anaposafiri kwenda na kurudi likizo

xix. Kuvaavu ya kofia, viatu vyagorofa, na mapambo yoyote, kama pete, mkufu, rozari, tasibihii, na bangili.

xx. Kutokuwa msafi wa mwili na nguo.

xxii. Marufuku kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa

- a) Ofisi ya walimu (staff room)
- b) Ofisi za shule
- c) Maabara
- d) Jikoni
- e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

xxiii. Sehemu zifuataao ni marufuku kabisa kutembelea.

- a) Vilabu vya pombe
- b) Kumbi/ nyumba za starehe
- c) Nyumba za kufikia wageni (guest house)

## **UTHIBITISHO WA MZAZI/ MLEZI**

### **KUHUSU TABIA NA MWENENDO WA MWANAFUNZI**

Mimi.....mzazi/mlezi  
wa mwanafunzi ..... ambaye  
amechaguliwa kuje na shule ya Sekondari Angaza kidato cha kwanza mwaka 2021.

- I. Nimekubali/sikubali mwanangu asome katika shule hii.
- II. Natii/sitatii na kumhimiza mwanangu kutii/kutotii sheria zote za shule kwa mujibu na kanuni na taratibu kama nilivyofahamishwa na uongozi wa shule.
- III. Nakubali/sikubali mwanangu kuadhibiwa kwa mujibu wa taratibu endapo atvunja au kukiuka sheria za shule.
- IV. Wakati wote mwanangu atakapo kuwa shule (mwanafunzi) hana ruhusa za kwenda kwenye nyumba za wageni, maeneo ya ulevi, kumbi za cinema na muziki.
- V. Naahidi kumpatia vifaa vyote vinavyohitajika kwa wakati.
- VI. Naahidi kumleta shulenii kwa wakati.
- VII. Naahidi kushirikiana na walimu katika kufatilia maendeleo ya mtoto kitaaluma.
- VIII. Naahidi kuhudhuria vikao vyote pindi nitakapohitajika.

#### **KUKUBALI SHERIA ZA SHULE**

##### **A: SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Jina la mwanafunzi.....

Tarehe ya kuzaliwa.....

Uhusiano (undugu, mlezi, baba, mama, mjomba, kaka n.k).....

Mimi .....

- a) Nikiwa mwanafunzi wa shule hii nakubali Umma wa Nchi ya Tanzania ndo ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kutumikia Nchi katika maendeleo yake.
- b) Hivyo naahidi kwamba nitajibidiisha hapa shulenii na pia nimalizapo shule ili kutimiza shabaha hiyo, nakubali na kuahidi kwa hiyari yangu mwenyewe na nitatii sheria za shule na amri zote nitakazopewa iwapo nitakiuka, sheria za shule zitachukuliwa hatua zake

## **B: SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

**Mimi.....**

..... ambaye ni Mzazi/mlezi wa mwanafunzi tajwa hapo juu, naahidi kutoa ushirikiano mzuri na uongozi wa shule katika kumlea mwanangu.

Nitakuwa tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala la nidhamu ya mwanafunzi na kwamba nitakuwa tayari kukubaliana na adhabu itakayotolewa iwapo mwanafunzi atakuwa amehusika na utovu wa nidhamu.

**SAINI YA MZAZI/MLEZI.....**

**TAREHE:.....**

### **MKATABA WA MAKUBALIANO BAINA YA MZAZI, MWANAFUNZI NA SHULE YA SEKONDARI YA ANGAZA**

Shule ya Sekondari Angaza kama zilivyo shule nyingine zote zilizosajiliwa kisheria kutoa huduma katika jamii ya serikari ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inataratibu na sheria zinazotumika kuiongoza shule.

Serikali ya awamu ya tano, kupitia waraka wa namba 5 wa ELIMU MSINGI BURE umekusudia kuhakikisha wanafunzi wote wanasoma bila vikwazo na wazazi na jamii kwa ujumla kuwasimamia katika usomaji wao.

Kupitia waraka wa serikali, shule ya Sekondari Angaza inatekereza majukumu yake yote yaliyoagizwa na serikali ya kumfundisha mwanafunzi ili kuweza kufaulu na kutopata sifuri. “DIVISION ZERO” katika mitihani ya kidato cha pili na cha nne.

**LAUS J. MCHOPA**

.....

**MKUU WA SHULE**

**SAINI YA MKUU WA SHULE**

## **TAMKO LA MWANAFUNZI**

Mimi.....mwanafunz i wa kidato cha kwanza 2021 hapa Shule ya Sekondari Angaza ninafundishwa/ kuandaliwa kufanya mtihani wa kidato cha pili/nne. Ninaahidi kuzingatia, kusikiliza, kufanya mitihani na mazoezi yote, na kufaulu katika masomo yangu yote na sitapata division four. Nikifeli mitihani hiyo kwa kupata DIVISION FOUR itakuwa uvivu na uzembe wangu mimi kwa kuwa nimefika kidato cha kwanza, tatu, kwa kuwa ninasifa na uwezo wa kusoma kwa sababu nilifaulu mtihani wa darasa la saba kutokana na juhudhi na uwezo wangu wa kusoma. Nikifeli niwajibishwe.

.....  
Saini ya mzazi/mlezi

.....  
Tarehe

## **OFISI YA MTENDAJI WA KATA.**

.....  
Saini ya Afisa Mtendaji Kata  
Muhuri .....  
Tarehe

## **TAARIFA MAALUMU YA KUHUSU MWANAFUNZI**

### **SEHEMU: A**

Jinakamili (HERUFI KUBWA).....  
Tarehe ya kuzaliwa.....  
Anwani ya nyumba.....  
Namba ya simu.....  
Kata.....jina la mtendaji wa mtaa.....

### **SEHEMU B**

Jina la baba/mlezi.....Namba ya simu.....  
Jina lmama/mlezi..... Hai/amefariki  
Kazi ya mama/mlezi .....Namba ya simu .....  
Hai/amefariki

**SEHEMU C**  
Taarifa za ndugu wa karibu

JINA LA NDUGU	UHUSIANO	KIWANGO CHA ELIMU	NAMBA YA SIMU

**SEHEMU D**  
Michezo/Sanaa nayoipenda

JINA LA MCHEZO	SHULE	TOKA MWAKA	HADI MWAKA

**SEHEMU E**  
Kazi yoyote/uongozi aliwahi kufanya

KAZI/CHEO	SHULE	TOKA MWAKA	HADI MWAKA

- I. Ninaahidi kuwa na tabia nzuri mchapa kazi na mwnyebidii ya masomo
- II. Nitafuata taratibu na sheria nitakazoelekezwa nitakapoenda kinyume na sheria ichukuliwe mkondo wake.
- III. Utoro kwangu mwiko

Saini ya mwanafunzi.....  
 Sahihi ya Mzazi/Mlezi.....  
 Tarehe .....